

## **TAARIFA KWA UMMA**

### **WITO WA MAONI YA WADAU KUHUSU MAOMBI YA LESENI KUTOKA MAMLAKA YA MAJI NA USAFI WA MAZINGIRA TURIANI**

Mnamo tarehe 15 Agosti, 2016, Mamlaka ya Udhhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA), ilipokea ombi la kupatiwa leseni kutoka Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Turiani (TURUWASA). Leseni inayoombwa ni ya kutoa huduma za majisafi na majitaka katika mji wa Turiani.

Mamlaka ya Maji Turiani ilianzishwa kwa tangazo la serikali namba 336 lililotolewa tarehe 30 Disemba, 2016, na kupewa majukumu ya kutoa huduma za majisafi na usafi wa mazingira katika mji wa Turiani. Mamlaka ya maji Turiani ilianza kufanya shughuli zake rasmi mwezi wa Novemba, 2015. Ofisi za TURUWASA zipo katika mji mdogo wa Turiani, uliomo katika wilaya ya Mvomero. TURUWASA iko katika daraja la C la Mamlaka za majisafi na usafi wa mazingira.

Yafuatayo ni maelezo kwa kifupi kuhusu mamlaka ya majisafi na usafi wa mazingira Turiani;

#### **1.0 Jina na Anuani:**

Mamlaka ya Maji na Usafi wa Mazingira, TURIANI  
Soko la Ndizi, Mtaa wa Rest House, Kichangani,  
S.L.P 663,  
Turiani-Morogoro,  
Tanzania

#### **2.0 Maelezo ya Leseni:**

Mamlaka ya Maji na Usafi wa Mazingira, Turiani, imeomba leseni ya kutoa huduma za majisafi na usafi wa mazingira mjini Turiani. Eneo la huduma ambalo, mamlaka inatakiwa ilihudumie ni mjini Turiani, wilaya ya Mvomero, mkoani Morogoro. Mipaka ya eneo hilo ni kama ilivyotafsiriwa katika Agizo lililochapishwa na Waziri mwenye dhamana wakati wa kutangaza Mamlaka.

#### **3.0 Miundombinu ya Majisafi na Majitaka**

Vyanzo vya maji vinavyotegemewa na TURUWASA ni mto Mvaji, wenye uwezo wa kuzalisha mita za ujazo 3,245 za maji kwa siku. Miundombinu ya muombaji, inajumuisha, matanki manne ya kuhifadhi maji, yaliyojengwa kwa zege, matanki 20 ya palastiki, yote kwa pamoja yana uwezo wa kuhifadhi mita za ujazo 665. Aidha, miundombinu hiyo, inajumuisha, mtandao wa kusambaza majisafi wenye urefu wa kilomita 47. Muombaji

hana mfumo wa kuondoa na kusafisha majitaka.

#### **4.0 Umliki**

Mamlaka ya Maji na Usafi wa Mazingira Turiani, inamilikiwa kwa asilimia 100 na Serikali ya Tanzania.

Kulingana na kipengele cha 19(2) cha Sheria ya EWURA, sura ya 414, EWURA imeanzisha mchakato wa kukusanya maoni juu ya uhalali wa maombi hayo ya leseni.

Mtu yeyote mwenye maoni au pingamizi kuhusiana na maombi tajwa hapo juu afanye hivyo kwa maandishi na kuwasilisha EWURA kwa anwani iliyotajwa hapa chini kabla ya saa 11 jioni ya tarehe 24 Aprili, 2017. Nyaraka za maombi hayo zinaweza kuoneshwa kwa mtu yeyote, kwa maombi maalum ya maandishi kwa anuani iliyooneshwa hapa chini.

**Mkurugenzi Mkuu,  
Mamlaka ya Udhhibiti wa Huduma za Nishati na Maji,  
Ghorofa ya 7, Jengo la LAPF Pension Fund,  
Mkabala Kijiji cha Makumbusho, Kijitonyama  
S.L.P 72175, Dar es Salaam,  
Simu: +255-(022) 2923513  
Nukushi: +255-(022)-2923519  
Barua pepe: [info@ewura.go.tz](mailto:info@ewura.go.tz) Tovuti: [www.ewura.go.tz](http://www.ewura.go.tz)**